**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**21 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA - TAREHE 21 MEI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**364 MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanzisha Vijiji vipya kwenye maeneo ya Songea, Mkamani, Kwaluma Masimba na Sekioga – Korogwe Vijijini.

**365 MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha maboma yaliyojengwa na Wananchi katika Mkoa wa Songwe.

**366 MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Kijiji cha Negero – Kilindi.

**367 MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Walimu wa Kike katika Shule ambazo hazina Walimu wa Kike Wilayani Chemba.

**WIZARA YA MAJI:**

**368 MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha mfumo wa maji taka Kiwanda cha A - Z ili kuondoa changamoto ya Wananchi wa Kata ya Olmot – Arusha.

**369 MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Miradi ya Maji katika Wilaya ya Kyela itakamilika.

**WIZARA YA KILIMO:**

**370 MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mawanda ya Mradi wa Bonde la Mto Ngono lililofanyiwa upembuzi yakinifu ili liweze kuendelezwa na lini ujenzi wa Mradi huo utaanza.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**371 MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itatokomeza uvuvi haramu katika Ziwa Tanganyika.

**WIZARA YA UJENZI:**

**372 MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali italipa fidia na riba kwa Wananchi wa Manyara Kibaoni Wilayani Karatu waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Manyara.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**373 MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, kwa nini Kampuni za CCECC na YAPI MARKEZI zinazojenga SGR Bukene zinatoa ajira zisizohitaji ujuzi kwa Vijana wanaotoka nje ya Bukene.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**374 MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Magari kwa Jeshi la Polisi Malinyi ili liweze kutoa huduma stahiki kwa Wananchi.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**375 MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali haioni haja ya kukifufua Kiwanda cha Pamba na Mafuta Kasamwa kwa kuwa hivi karibuni nchi ilikabiliwa na uhaba wa mafuta.

**WIZARA YA AFYA:**

**376 MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kipi chanzo mahsusi cha fedha za kugharamia huduma ya afya kwa Mama Mjamzito na Mtoto chini ya miaka mitano.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**377 MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itafikia makubaliano na Makampuni yanayotoa huduma ya *Internet* kwa *Satellite* Duniani kutoa huduma hapa nchini.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** — **BARAKA I. LEONARD**
**21 MEI, 2025** — **KATIBU WA BUNGE**